*JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA*

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

*(Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa shule,*

Mkuu wa shule

S.L.P 63

UramboTabora

***Simu*:**

**0763441838/0672345855-** MKUUWASHULE

***0743575922-*** SIMU YA OFISI

***0754535949***-MAKAMU MKUUWA SHULE

Kwa.........................................................................................

S.L.P.......................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MARGARET SITTA MWAKA 2026.**

Uongozi wa shule ya Sekondari ya Wasichana Margaret Sitta inayo furaha kubwa kukupongeza kwa kuchanguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza kwa mwaka 2026.

Shule ya Sekondari ya Wasichana Margaret Sitta ipo Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Urambo,Tarafa ya Urambo, Kata ya Urambo. Shule ni ya Wasichana ya Bweni kitaifa.

Shule ipo kilometa 2.5 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Wilaya Urambo..Kutoka stendi hadi shule utapanda bodaboda/pikipiki au Bajaji hadi shuleni kwa nauli ya shilingi Elfu mbili (Tsh 2000/=).

Muhula wa masomo unaanza tarehe 13/01/2026, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe 13/01/2026 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 20.01.2026.

Utakapokuwa umetimiza mahitaji yaliyomo kwenye fomu zilizoambatanishwa pamoja na maelekezo haya, utapokelewa na kuingizwa katika kitabu cha Usajili wa Wanafunzi.

Wakati wakupokelewa unatakiwa kujana vitu vifuatavyo:-


i. Fomu ya kujiunga na shule (***Joining Instruction form***)

ii.. ***Medical examination form***

iii.Fomu ya kukubali kujiunga na Shule

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MARGARET SITTA.**

*SCHOOL MOTTO*: "***BELIEVE BIGGER, AIM HIGHER***"






## 1.SAREZA SHULE.

I. Sare ya shule hii ni suti na tai **(AWE NAZO MBILI** )Sketi ya vyumba vyumba vyeupe na dark blue.( iwe na urefu wa nchi 5 kutoka magotini) rinda box.Kwa waislamu wanaovaa hijab sketi iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu,koti jeupe lenye michirizi ya kitambaa cha sketi mikononi na kwenye kola.Shati jeupe la mikono mifupi.(kama inavyoonekana pichani )



II. Kwa waislamu rangi ya Hijab ((KIJUBA) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi isifunike tumbo na kisiwe na urembo.

III. Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi jozimbili(2),kisiwe na shingo ndefu kama buti,

IV. Soksi ndefu nyeupe (stoking free size)jozi za kutosha.

V. Gauni mbili(2) rangi ya kijivu kitambaa kizito za kushindia/Shamba dress mshono wa solo ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu,kwa waislamu hijabu ya kushindia rangi ya maroon kisiwe na urembo.

VI. Sweta rangi ya dark blue

VII. T-shirt mbili (2) light blue yenye kola nyeusi.

VIII. Tracksuit dark blue yenye michirizi mweupe isiyo na kofia

**ZINGATIA:** Vipodozi vya aina yoyote haviruhusiwi,Wanafunzi hawaruhusiwi kusuka nywele, kuvaa hereni,Mkufu (chain) pete , body splashi udi au marashi yoyote . vyote ni marufuku..

**2.MAHITAJI MENGINE KWA WOTE.**

- Shuka mbili (2) rangi ya pink,mto wakulalia na neti pembe nneya rangi ya blue.
- Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe visiwe vya plastiki )
- Godoro **2.5 x 6** (aje nalo).
- .Ndoo 2 lita 10 zenye mifuniko na galoni la lita 5 kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa. kwa matumizi binafsi.
- Jembe 01 lenye mpini
- Fyekeo 01
- Fagio ya ndani 01 (soft bloom)
- Fagio la nje 01 (Hard Bloom)
- Kitenge/kanga mbili, kandambili,kitana na kioo kidogo
- Tochi ndogo ya betri au sola taa (Haruhusiwi kuja na tochi,taa au pasi ya umeme.)
- .Faili 01 la plastiki.

**3.VIFAA VYA MICHEZO**

- T-shirt rangi ya kijivu isiyo na kola
- Raba nyeupe jozi moja.
- Soksi za michezo rangi nyeusi jozi mbili

**ZINGATIA:**T-shirt zisiwe na maandishi ya aina yoyote,

**4.VIFAA VYA DARASANI**

- Daftari kubwa angalau12. (counterbook-kuanzia quire three) na daftari ndogo ya Msomi -12).
- .Kalamu za wino za kutosha.

  Ream paper A4-02 kwa mwaka
- Kalamu za risasi za kutosha.
- Kila Mwanafunzi anashauriwa kununua angalau kitabu kimoja kwa kila somo-kiwe kitabu cha TIE)
- Mkebe wa hisabati (Mathematical Set).
- Graph pad
- Mathematical figure/4-figures

Tafadhari soma kwa makini maagizo/ maekekezo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.Vilevile umeambatanishiwa fomu A na B nazo zinatakiwa kujazwa kabla ya mwanafunzi kuripoti Shule

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya Sekondari Wasichana Margaret Sitta inaendeshwa kwa mujibu wa **sharia ya Elimu Na.25** ya **mwaka1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na.10 y**a **mwaka 1995.**Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara·ya Elimu,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-Tamisemi yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kufika shuleni:-

a. Heshima kwa viongozi,wazazi,wanafunzi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio kama itakavyokuwa imepangwa (preparation time)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote katika Maisha yako ya shule.
f. Kuvaa sare ya shule kikamilifu wakati wote uwapo shule.
g. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h. Kutunza mali za shule/umma.
i. Kuheshimu nembo zaTaifa kama vile wimbo waTaifa,bendera ya Taifa n.k

**MUHIMU**

- **.** Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile, na hakuna mtumishi yeyote yule anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa, ni marufuku mwanafunzi kulala na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa, kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu cha Mkuu wa shule(Msiba au ugonjwa)
- Mwanafunzi aje na **BIMA YA AFYA** na kwa mwanafunzi ambaye hana bima ya afya gharama za matibabu atashughulika mzazi au mlezi wake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini au kumshawishi mwenzake kubadili dini wawapo shule.
- Mzazi/Mlezi ambaye atakuwa amesajiliwa katika daftari la wazazi siku ya kumleta mwanafunzi shuleni ndiye atakayeruhusiwa kuja kumtembelea mwanafunzi huyu siku ya (Visiting Day) ambayo ni kila jumapili ya mwisho wa kila mwezi.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**


**a.** Wizi wa aina yoyote ndani au nje ya shule
**b.** Uasherati,kuwadi , ushoga na usagaji.
**c.** Ubakaji
**d.** Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine, mirungi, n.k
**e.** Kupigana au kupiga
**f.** Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
**g.** Kudharau bendera yaTaifa.
**h.** Kudharau wimbo waTaifa.
**i.** Kubeba mimba na kutoa mimba au kusaidia mtu kutoa mimba.

**j.** kuolewa
**k.** Kugoma au kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule
**I**.Kukataa adhabu kwa makusudi.
**m**.Kumiliki **SIMU** ya mkononi, **RADIO na vifaa vya kielektroniki.**
**n.** Kwenda kwenye kumbi za starehe na nyumba za kulala wageni
**p** . Kufanya jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu
**q.** Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA.**

Sahihi na Muhuri wa Mkuu wa shule






**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli( wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahutihuti hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE KABLA YA KUWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA.

WASILIANA NA NAMBA ZILIZOKO KATIKA FOMU HII.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MARGARET**

**SITTA. FOMU: A**

Nenda na fomu hii kwa mganga wa serikali akupime na kukujazia

Tarehe..........................
Mganga wa wilaya*I* mkoa……………………….,
S.L.P......................

**MEDICAL CERTIFICATE**

Jina la mwanafunzi………………………………………………………………………………..

1. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona amepatikana na ugonjwa wa …................................... …………………………………………na nimemtibu ipasavyo.
2. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona na ugonjwa hawezi kusoma kwa sababu ya………………………………………………………………………………………
3. Nimemwona ana mimba/hanamimba. (**kata panapohusika**).

   NB: Tutakayemtilia mashaka tutampeleka hospitali kwa daktari wa hapa wilaya ya Urambo.

4. Afya yake kwa ujumla,

   a. Kifua..........................................................................................
   b. Macho........................................................................................
   c. Masikio.....................:.................................................................
   d. Kilema chochote,kitaje…………………………………………………
   e. Akili............................................................................................
   f. Mkojo.........................................................................................
   g. Choo (stool)................·...............................................................
   h. Mimba...............·...........................................................................

Sahihi ya Mganga...................... Muhuri.................. Tarehe ..........:.......

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO.**

SEKONDARI YA WASICHANA MARGARET SITTA,
S.L.P 63.
URAMBO-TABORA

**FOMUB: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

1.Jina la mwanafunzi ..........................................................................

2.Jina la mzazi/mlezi ...........................................................................

Mimi..................................................................Nimekubali kuwa mwanafunzi wa shule ya Sekondari Wasichana Margaret Sitta,nimesoma kwa umakini sheria na taratibu zote za shule na kuwa nitazizingatia na kuzifuata wakati wote niwapo shule. Aidha nitajituma kwa bidii katika masomo yangu katika kipindi chote niwapo shuleni.Nikiwa na maoni au Malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia nataratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi...........................................tarehe.........................

Mimi........................................................................Nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………………………………………………………………………...
Naahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu
Kama mzazi/mlezi wa mtoto na kushirikiana na Uongozi wa shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi...................................Tarehe.................................